

**CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION**

**CKRC**

**VERBATIM REPORT OF**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, AMAGORO  
CONSTITUENCY AT MALABA TOWN COUNCIL**

**ON**

**1<sup>ST</sup> AUGUST 2002**

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, AMAGORO CONSTITUENCY, PUBLIC HEARINGS HELD AT  
MALABA TOWN COUNCIL ON 1<sup>ST</sup> AUGUST 2002**

**Present**

Com. Pastor Zablon Ayonga  
Com. Dr Abdirizak Nonow  
Com. Mutakha Kangu

**Secretariat Staff in attendance**

Samuel Wanjohi - Programme Officer  
Hellen Namisi - Asst. programme Officer  
Grace Gitu - Verbatim recorder  
Charles Ekisa - District coordinator

**The meeting started at 10.00am with Com. Pastor Ayonga in chair.**

**Mr. Charles Angesu Ekisa:** The district Commissioner Teso the OCPD Teso chairman Teso county council, chairman Malaba Town council, the leaders other leaders of the district mama bibi na mabwana hamjambo. Nafikiria tuanze mkutano wetu kwa maombi tuweke mungu mbele yetu asubuhi ya leo. Tafadhali Reverend Lawi Emukule kama unaweza kutuwekea mbele ya mungu tafadhali tusimame.

**Rev Lawi Emukule:** Natuombe; Baba Mwenyezi Mungu muumba wa vitu vyote na hasa muumba wa mtu aliyefanana nawe na akawa na akili kama yako. Baba tuna kushukuru tunakutukuza kwa ajili ya wema wako umetupa siku hii siku nzuri katika wilaya hii ya teso na kwa jamii yote ya teso. Mungu tume kuja pamoja kukutana na Commissioners wako ambao umewatuma kwa ajili ya nchi yetu na kwa ajili yetu mungu ni wewe uliye tangulia ukandika amri kumi na katika amri kumi mungu ulijumlisha mambo yote yanayio husu mwanadamu katika dunia hii. Na kutokana na hayo amri kumi mungu ulijumlisha mambo yote yanyohusu mwanadamu kuhusu dunia hii. Na kutokana na hayo amri kumi mungu mwanadamu amejijenga na ameendelea. Na hata wakati huu tuko mbele yako kwa ajili mungu tunataka kuendelea. Tunaomba wape hawa viongozi hasa mwenyekiti akayo ongoza mkutano huu na Commissioners wengine na wasemaji wa jamii hii ya teso ili kwamba mungu yale yote tutakayo sema yawe ya manufaa kwetu na jamii itakayo kuja na hata kwa maisha yetu yote tukitakapo ishi hapa duniani.

Mungu uliyahidi ukasema chochote utakacho omba kwa imani utatupa na imani yetu ni kwamba bwana utaongoza inchi yetu na utaongoza watawala wetu na katiba hii utakao uyandika mungu itakuwa katiba itakayo leta amani na umoja katika nchi yetu ya kenya. Na tuna omba hayo tukiwa na imani utatufanyia kwa mapenzi yako. Na nina omba yote ya fike kwako bwana katika jina la yesu kristu aliye bwana wetu.

**Mr. Charles Angedu Ekisa** Hamjambo tena mimi kwa majina ninaitwa charles Angedu mimi ndio district coordinator wakati hii ya Commission najua ya kwamba tumekua tukikutana mara mingi kwa kazi hii kwanzia wakati wa elimu mpaka wa sasa. Kwa leo tuko na shughuli muhimu vile mnavyo jua kwamba Commissioners wetu wako hapa kuchukua maoni yetu kuhusiana na yale ambayo sisi kama wana Kenya tunge penda iwe au yawe katika katiba mpya tunayotaka kuunda. Na kwa sababu hiyo sisi wote tume kusanyika hapa na ninge wawomba kwa siku ya leo iwe tu ni kwa sababu ya hiyo ndio tume kusanyika hapa ili kukamilisha kazi hiyo. Ninge omba nyinyi kwamba kuna programme kidogo hapa wale ambao hawajapata tafadhali kuna mmoja wetu anapeyana programme ya siku. Na nilikuwa nataka tu kuwambia ya kwamba kutakuwa na nafsi kwa wale ambao wako tayari kutoa maoni yao. Natumai kwamba kila mmoja atapata nafsi lakini tumeonelea kwamba tungekuwa na utaratibu fulani ambayo imewekwa katika programme hii.

Tumeweka hio utaratibu katika hiyo programme na tutaifuta hivyo. Pengine tu kuanza ingekuwa vizuri tupatie wenyeji ambao ni Malaba town council wangetuanzishia programme hii. Sitaki nisome hayo yote kwa sababu yako katika mandishi, na pengine kwa kifupi tu kwa sababu tuko hapa kwa sababu ya kurekebisha katiba yetu katika wilaya teso tumesaidiana vilivyo sana katika hii kazi pamoja provincial administration yetu katika hali na mali tangu mwanzo mpaka wakati huu tuko na district Commissioner wetu hapa ametusaidia kabisa. Na vile tulivyo endesha mambo ya elimu kwa rahia civic education hiyo kazi iliendelea vizuri tuliweza kufikia watu karibu elfu kumi katika katika mikutano zetu na tunatumaini ya kwamba hiyo elimu imewaweka katika hali nzuri ya hii leo nyinyi kutoa maoni yenu vilivyo. Na ukipata nafasi tafadhali yakuja hapa mbele tafadhali uweze kuja hapa mbele ninge omba kwanza kabisa ujitambulisha useme wewe ni nani ikiwa una pengine wewe ni msimizi wa shirika fulani uweze kutaja hiyo shirika ili ijulikane waziwazi kwamba maoni yale ambayo unaenda kutoa ni pengine ni maoni ya kikundi fulani ijulikane waziwazi hivyo. Kama ni maoni ya wewe binafsi useme hivyo ni maoni binafsi. Na ninge omba kwamba tafadhali maoni haya tuweze kuweka katika ile hali ya kuwa wazi sio kuanza kupiga story kando kando sema vile wewe unafikiria ili ieleweke maramoja. Tume elewana hivyo? Ndio. Na ikiwa mmoja wetu anapeana maoni yake tafadhali tumpatie nafasi sio kwamba vile mtu amesema sio vile wewe unafikiria ni vile yeye huyo mtu anavyo fikiria. Na sisi wote kama wanakenya tupeane nafsi kila mmoja aweze kutoa yale yote yeye ako nayo kwa roho. Na sitaki kuchukua mda mwingi ninge karibisha mwenyekiti wa kamati ambayo imekua ikiendesha mambo ya urekebishaji wa katiba katika district yetu. Mnajua kwamba hiyo kamati iko na watu kumi wamekua wakienda kila pahali katika district yetu wakati hii. Tafadhali ninge patia chairman wetu wa CCC nafsi aseme neno moja ama mbili. Tafadhali karibu .

Commissioners wetu ambao ni wageni wetu wa siku, bwana district Commissioner wetu ambaye yuko pamoja nasi, wenye kiti wa Malaba town council wenye hall hii teso count council ambao tuko pamoja nao halafu viongozi wote kwa jumla ambao tuko pamoja nao alafu viongozi wote kwa jumla ambao tuko pamoja na viongozi wa kinyumbani hapa na sehemu fulani fulani alafu baba Emori Mori ambaye yuko pamoja nasi kama viongozi wa hapa. langu litakuwa jambo fupi kabisa. Kwa sababu yake siku ya leo si ya committee yetu, siku ya leo ni yenu, yaani siku ya wakaaji wa Teso district kupeana maoni yenu. Kwa hivyo kwa ufupi Commissioners langu ni kuwakaribisha hapa uwe uhuru na uwe tayari kusikiza maoni yetu, pengine maoni yetu mengine yatakuwa makali au rahisi au namna gani na ninavyojua nyinyi ni watu ambao mumejitia maoni mbali mbali katika jamuhuru yetu, we have a feeling you will accommodate everything as it will come.

Kwa hivyo kwa upande huo na kwetu sisi kama wenyeji wa nyumbani, huu ni wakati wetu ambao ni maalum kabisa, ambao ni lazima tupeane maoni yetu yote kwa sababu kesho tusije tukaseme pengine tulisahahu hii, pengine tungepeane hii kwa sababu itaingishwa kwa Sheria mabo twajua sote itatusaida kwa wakati huu na vizazi vijazo. Kwa hivyo kwa hayo mengi ambayo nimeyasema kwa sababu tunawakati uliomfupi, langu tu ni kuwashukuru kwa kuja na kwa sasa nitarudisha hii jambo kwa bwana District Commissioner wetu ambaye atakuja kuwakaribisha Commissioners wetu pamoja na wengine. Bwana District Commissioner.

**Bw. D.C:** Asante sana bwana Chairman, Commissioners, ambao mumeleka hapa leo, ma ofisa wezangu wa serikali viongozi wa tabaka mbali mbali, Hamjambo. Kazi yangu ni fupi sana, leo nikukaribisha Commissioners kuja hapa kwetu tunashukuru mumeleka nafasi ya kuja ili kuchukua maoni ya viongozi na wananchi ili kushiriki katika marekebisha ya Katiba. Langu muhimu zaidi ni kuwaomba wananchi na viongozi ambao wako hapa leo siku hii kweli ni yetu, ma Commissioners wako hapa ili tuwapatie maoni yetu lakini yangi ni kuongea kuhusu utaratibu. Mara kwa mara unakuta tunajirudia rudia sana mpaka mwisho tunakuta tunafika saa kumi na mbili na yale ambayo tumezungumza pengine ingemaliza ma saa mawili Matatu. Kwa hivyo mwezako akizungumza huna haja kurudia tena kusema mimi namuunga mkono unarudia yale amezungumza tena. hiyo huwa inamaliza wakati mwingi sana.

Kwa hivyo tafadhali tujaribu kuongea yote ambayo tuko nayo, mwingine naye aongee yake tumpatie heshima badala ya kumuambia wewe kaa, hiyo pia inapoteza wakati. Kwa hivyo tuheshimiane na tuongee yale tuliyo nayo tusirudie. Hiyo itatupatia nafasi ya kuongea mengi zaidi na kuuliza maswali baadaya kwa sababu kulingana na programme hii ni vipindi viwili. Kuna wale ambao wameandika wako na memorandum tofauti tofauti na wengine ni wale ambao watapewa maoni yao ya kibinafsi wakisimama ambao haikuandikwa. Tukichukua muda mrefu kuongea mambo ya yale maoni ambayo yameshaandikwa wale ambao wana maoni yao ya kibinafsi hawatapata nafasi. Na kama umekuja memorandum yako, tungekutazamia utupatie ile tunaita executive summary. Kama ni page kumi utosomee page mbili peke yake ambayo umeandika kando kuhusu document yote.

Commissioners hawa kazi yao ni kusoma hiyo yote kwa hivyo leo watachukua hayo maoni wataenda nayo lakini ukisema unataka usome page ishirini. Tarifa ya habari yenyewe ni dakika kumi na tano, na wewe sasa kama utaongea nusu saa na tuko wengi unafikiri tumaliza kweli leo. Kwa hivyo tafadhali kama uliandika tunaamini kuwa wewe zile page zako hamsini si ni wewe uliandika, kwa nini zikushinde kuongea kwa dakika tano? Si zako basi kwa sababu kama ulichukua kalamu na karatasi kuandika ukurasa hamsini you should be able to summarise it for us. yangu ni hiyo tu, ni kuwaomba ili tuweze kusikiza wengi zaidi kuliko kusikiza wa tatu na siku imeisha.

Commissioners mimi yangu ilikuwa ni hayo, muwe huru, be as free as possible kwa sababu it is not every day the Commissioners will get an opportunity to come down here. pengine bwana chairman kulikuwa na oversight kidogo kwa sababu hapa ni kwako nyubani lakini nitakupatia nafasi utukaribishe tena kwako zaidi lakini usilete hotuba.

**Samson Olubayi:** I don't know whether I am expected to present my memorandum. Asante sana. Waheshimiwa Commissioners ambao wako hapa nasi, District Commissioner wa Teso OCPD, chairman wa Malaba Town Council sisi wananchi kwa jumla Hamjambo. Mimi ningependa kwa niaba ya wafanyikazoi wa Malaba Toown Council, councillors na wakaaji wote wa Malaba Town Council kirasimi kabisa kuwakaribisha nyinyi nyote hapa haswa Commissioners wetu, tunajua Commissioner Mutakha hapa is not there first time they are coming here, today is their third time if I am nor wrong. Kwa hivyo ningependa kusema karibuni Malaba Town council na Malaba Town council ni karibu seshemu moja, is a quarter of Teso

district. Kwa hivyo mjisikie nyumbani na we wish that tutakaa hapa mpaka pengine kesho, karibu sana. Asante.

**Bw. D.C:** Asante Bwana Chairman. Kuna kiongozi mwingine hapa atasema mimi sipendi yeye na mimi napenda kila kiongozi. Bwana Chairman amuka tu na wewe uonekane wa county council. Huyu ni Chairman wa County Council. Sasa unajua ukipatia Town Council ukiwacha County Council wanasema “mimi najua tu” . kwa hivyo ningependa kurudisha kifaa hiki kwa coordinator ili tuendelee na taratibu yetu asanteni sana.

**Mr. Charles Angedu Ekisa :** Thank you very much District Commissioner Teso. Sasa wakati huu nitakaribisha Commissioners wetu waweze kuchukua nafasi hii kuendesha programm ya kuchukua maoni yetu. Tafadhali.

**Com Pastor Ayonga:** Kwanza nimetaka kuwashukuru nyote kwa kufika kwenu hapa leo. Na mushkuru bwana DC na viongozi ambao wametukaribisha katika hall hii na jinsi ambavyo mumefika kwa wingi naona jumba kimejaa na wengine wamesimama kule. Na kwa hivyo kwa niaba ya Commissioners ambao tuko hapa, nachukua nafasi hii kwanza kwa kuwasalamu nyinyi nyote, Hamjambo? Ningalijua lugha ya Kiteso ningewasalimu kwa Kiteso lakini nafikiri at the end of the day I would have asked na nijue wateso wakisalimiana wana salamiana aje? Mbona huyu Mutakha Kangu hata Kiteso kinamshida na amakuwa hapa mara tatu. Lakini mimi nitafanya bidii at the end of the day nitawaambia kwa heti kwa Kiteso. Sasa sisi tumefurahia tumekuwa, we have zbeen looking forward for the day that we are to come here. wengine wetu this is a first time to come here lakini tunajua tuko kati ya ndugu na dada wetu wenzetu.

Na bila kupoteza wakati nataka kwanza niwajulishe wale tulio nao. Kwanza mimi ni pastor Zablon Ayonga, ni one of the Commissioners na nitakuwa mwenye kiti wa kikao hiki cha leo. Kando mkono wangu wa kulia nina Dr. Nunow, Commissioner yeye atakuja kuwapa salamu zake ambazo zinatoka North Eastern, mnaona kule ni mwisho wa Kenya na hapa ni mwisho mwingine wa Kenya, sio? Kwa hivyo leo yeye ataleta salamu zake ni nzito kwa maana pia zimetoka mbali na nitakuja kumpa nafasi awasalamie. Na commssioner Mutakha Kangu yeye ameshakuwa akiwasalimia lakini kila wakati napata salamu zake zinakuwa mpyia kila wakati. Na leo vile tuko Teso District naye nitampa nafasi awasalamia.

Na ninao pia wafanyi kazi kutoka secretariat yetu ambao wako hapa ambao wana kazi ya muhimu sana sana. Wapi ndugu Wanjohi? Huyu mnamuona huyu Wanjohi huyu ndio mkubwa wa mambo njisi yanavyo endelea. Yeye ni Programme Officer, na Programme Officer ana mambo ambaye anaangalia. Wapi lile lijitabu lako la kuweka memorandum? Munaona folder hiyo kqwa wale ambao mna memorandum, mnaona hata imeandikwa Amagoro, maana ya Amagoro ni nini? Ni forest, okay, na sisi ina maana yake kwa lugha yangu. Sisi inamaanisha ni miguu, moja tunaita *okogoro* ikiwa mbili tunasema Amagoro. Kwa hivyo mambo yana kuwa tofauti from time to time, unajua kugha zunapitana. Kwa hivyo yeye atakuwa akifanya kazi ya kuandikisha unapo toa maneno yako, ukimaliza hapa kutuambia tutakuambia enda kule, kule unaenda kujiandikisha. Memorandum yako utai-register kule na utaweka kidole ya kuthibitisha ni yako. Halafu tuna wasichana wawili hapa, ambao pia mmoja wao anaandika na mwingine ana kuile chombo cha kushika, kanda ile ya kushika maneno, leo hakuna neno la mtu litakalopotea hata

moja, hata mkiona Bwana Mutakha haandiki au si andiki au Dr, Nunow handiki, usije ukafikiri mbaona mimi nilipokuwa nikiongea ninaona hawaandiki kitu .

Hawa watu kweli wamechukua maneno yangu? Sisi kile chombo ndicho chenye maana, hata ukikohoa leo, kikohozi chako kitachukuliwa na siku ingine ukienda kukana kwamba si wewe uliosema tunasema lakini nani huyu alikuwa anakohoa, si ni wewe kwa hivyo tuna kitu ambacho kitakunasa vizuri sana na kwa hivyo tunapokuambia ukifika hapa tunasema sema majina yako, si kwamba hatukuona jina lako latika maandishi hapa, tunataka jina lako liingie katika kile chombo kinacho nasa maneno. Kwa hivyo hawa dada wawili watanasa maneno, wataandika maneno.

Nitawapa hawa ndugu zangu nafasi wawasalimu ndipo niwaambie kiti kingine ambaco tunaenda kufanya. Kwanza pengine tungeleta zile salamu ambazo zimetoka mbali sana kwa maana pengine zinamvunja mgongo mbona azidi kuwa na mzigo. Let me make it easier for hime. Dakitari, salamia watu toka North Eastern.

**Com. Dr. Nunow:** Asante sana Commissioner Ayonga, wananchi wa Teso, salama Aleikum? Yoga? Asanteni sana. Tuna furaha sana kuwa nanyi na nafikiri kwa upnasde wa tume wa kurekebisha Katiba tunaangalia kuchukua maoni yenu kama mtu ambaye anaenda kuvuna shamba, harvesting. So vile tumekuja ku harvest views zenu tuna matumaini tuwe na pamba harvest leo, harvest ambayo ni kubwa hamna mmea moja ambao itakuwa itakosa kupeana zao. Si ndio? Asanteni.

**Com Mutakha Kangu:** Watu wa Teso Yoga? Yoga? Mzee unaona najua. Mnajua huyu mzee nilimuambia wakati tulitoka upande huu wakimbie wakaona wanataka mahali pa baridi, wakasonga huko wakaharibu lugha. Si mnajua waluyia wanaita miguu *amagulu* na hawa wanaenda huko wanasema *amagoro*. Asante. Basi siku ya leo ni yenu tutasikiza nyinyi. asante sana.

**Com Pastor Anyonga:** Nitamuuliza Commissioner Kangu aweze kutuambia taratibu, kila pahali ambapo watu wanaenda kufanye kazi wanataka wajue taratibu, wajue huu ndio mwisho , huu ndio mpaka unachotakiwa kufanya. Tumetaka atuambie taratibu njisi ambayo mungeweza kufanya ili tuwe na njia moja ya kufanya vitu, tusije tukakosea kwa maana leo si siku ya kuuliza maswali, tulipokuwa tukifanya Civic Education tuli expose our selves to questpiopns and answers. Leo tumekuja jinsi ambavyo Dr. Nunow amesema to harvest. Unapo enda ku-harvest wakati wa kulima, kupanda sasa unaenda kukata na kuweka kikapu. Sasa tunataka kuwaambia njisi ya kukata na kuweka kikapuni. Ningemuuliza ndugu Mutakha Kangu atoe yale maelezo ya taratibu njisi ambavyo tutafanya na ninaamini sisi sote tutafuata hizo taratibu kwa maana zinatusaidia kwa kufanya upesi na kufanya more efficiently.

Kitu kingine kabla sijasahahu. Nataka nyote mkumbuke kwamba hapa leo hatukuja mkutano wa siasa. Tumekuja katika jambo ambalo ni a very serious matter. Tumekuja kukusanya maneno ya maana yatakayo tusaidia kutengeneza au kurekebisha Katiba yetu ambayo ndio maisha yetu, ambayo ndio kipawa tutampa watoto wetu na wajukuu wetu na vizazi ambavyo viko mbele. Ningeomba hivi ndugu zangu na dada zangu wa Teso kwamba hakuna kupiga makofi. Mkienda kotini mnapiga makofi? Na

ikiwa mtu amaesema jambo na limekuchoma kwa roho, pia tumetaka upoe tu, hayo ni maoni yake. Mwingine atakuja aseme hata kitu unasema moyoni unasema upuzi mtupu, lakini upuzi mtupu huo ni wa nani, ni wa yule. Kwako ni upuzi kwake si upuzi. Kwa hivyo tuheshimiane vizuri na tukiheshimiana tutafanya haraka. Utaona tunakwenda haraka na kila ambaye amekuja hapa atahudumiwa vilivyo. Kwa hivyo ndugu klangu nataka kwa kifupi utoe taratibu kabla sijaanza kuita watu kutoa maoni.

**Com Mutakha Kangu:** Asante Commissioner Ayonga. Nitaenda kwa haraka, mradi wa leo ama mkutano wa leo ni wa kuchukua maoni ya watu wa Amagoro, tutakuwa na mikutano tatu, leo tuko hapa, kesho tutakuwa Alupe na Jumatatu tutakuwa Amakura. Watu wa Amagoro constituency mumeapatiwa 3 venues.

Now tukichukua maoni nyote mnajua wa Kenya walisema wanataka Katiba yenye imetoka kwa watu wenyewe. Kwa hivyo tunataka kuchukua maoni kwa kila mtu, iwe wazee, wamama, vijana, walemavu, kila mtu na kila mtu apatatiwe nafasi ya kujieleza na vile pastor amesema hakuna haja ya kukanusha yale mwezako amesema kwa kuopiga kelele, unatulia, nafasi yako ikifika taweza kusema hukubaliani na yale mwenzako alisema na wewe unasema iwe namna hii. Hivyo ndio tutaenda sawa sawa. Na sababu ingine ya muhimu ni kwamba ni ikiwa mambo imekufurahisha unapiga mikono ama haikufurahishi unapiga kelele, utaweza ku- interfere na ile recording yenye tunataka tunase sauti ya kila mtu anazungumza, ndio baadaye tukikaa kuchunguza maneno tunaweza sikiza yote yenye ilitoka teso. Kwa hivyo tuonyeshe heshima, tuionyeshe tolerance ndio kila mtu ajieleze vile anataka.

Jambo la pili ni kwamba mkutano huu ni mkutano wa Tume ya kurekebisha Katiba, si mkutano wa Bwana DC, si mkutano wa Town council chairman, ni mkutano wa Commission na kwa hivyo kila mtu ajisikie uhuru asunumze yale anataka kuzungumza bila uoga. Kwa sababu kwamba DC yuko hapa, isikufanye ufikirie nikisema hivi bwana DC ataniuliza nilikuwa nikisema nini. Huko uhuru, usiogope Bwana Chief yuko hapa ama sub chief hata naye Chief asiogope DC yuko hapa, ni mradi wa wa Kenya wote walikubaliana kuna shida vile tunaendesha maneno yetu kwa hivyo tuchunguze tujue shida yenyewe ni nini, na suluhisho ni nini. Na ikiwa unakuja na maneno na urudi nayo nyumbani kwa sababu umeogopa hautakuwa unasaidia kusuluhisha shida. Na Bwana DC na watu wa serikali wote tumekuwa tukiwasiliana nao na wamejua so they will not cause you any problem, tupatie maneno yako. Hata ukitaka kusema we don't want provincial administration, just say so kwa sababu hayo ndio maoni yako. Usiwe na uoga and DC has assured us on that.

Now jambo la tatu ni kwamba maoni tunachukua kwa sehemu tatu. Namna ya kwanza ni wale wako na maandisha, written memorandum na hawataki kuongezea ama kuzungumzia hiyo maandishi. Unakuja pole pole kama uko na maoni ya aina hiyo, unapeana pale, kuna register wataingisha jina lako, utaweka sahihi na ikiwa unataka kuenda unaenda, ikiwa unataka kukaa kusikiza wengine unakaa unasikiza unakimia, hiyo ndio sehemu ya kwanza.

Namna ya pili ni kwamba kuna wale wako na maandishi lakini wanataka kuyazungumzia ama kuyaelezea hayo maandisha. Tutawapatia nafasi utakuja hapa mbele na uweze kuelezea hayo maandishi na si kusoma yote vile amesema, nikuulika yale ya

muhimu kwa sababu mwishoe tutasoma hayo yote na tuweze kuelewa. So utapatiwa nafasi ukimaliza tena unaweka sahihi palena unapeana hayo maandishi hapo.

Namna ya tatu ni watu wenye hawana maandishi yoyote na hao ndio tunasema lazima wapate nya kuzungumza leo kwa sababu tukienda bila kuwasikiza hatutakuwa na kitu tunaenda nao na hao pia nao watakuja hapa mbele waeleze mambo yenye wanaeleze tunaandika inanaswa na mtambo wa kunasa sauti ndio itachunguzwa tujue itakuwa namna gani.

Kwa wale wako na maandishi na wanataka kuyazungumzia tunaomba ujaribu tutakupatia dakika tano ku-highlight the main issues in the memorandum. Kwa wale wenye hawana maandishi tunawapatia dakika kumi ya kuzungumza yale wako nayo. Lakini tuna discretion. Tunaweza anagalia mtu tuone huyu ni opinion leader na amebeba maneno ya watu wengi, tunaweza muongeza muda aelezee sawa sawa kwa sababu pengine anaeleza kwa niaba ya wengine na saa ingine tena mapema tunaweza ona watu hawajakuwa wengi tunaweza ongeza muda. Lakini muda ikianza kuishi inanza kufika jioni, inaweza tubidi tuanze kupunguza muda kwa sababu tunataka kusikiza kila mtu. na tena baada ya wengi kusungumza itafika kiwango uone yale ulikuwa unataka kuzungumza yamesha zungumzia, hakutakuwa na haja kila mtu akuje kurudia the same thing. Unaweza kuja to gove what has not been mentioned ama kupeana a different perspective ya yale yamezungumziwa so ndio tuweze kuenda haraka na kupatia kila mtu nafasi. So hiyo muangalie halafu you note mjue itakuwa namna gani.

Mkutano haswa unatakikana uanze saa mbili na unaisha saa kumi na mbili isipokuwa tumechelewa leo kidogo lakini tutajaribu kuenda tuone itakuwa namna gani.

Ukimaliza kuzungumza, sisi tutakuwa na swali moja ma ambili ya kufafanua yale umetuelezea na ikiwa uko na majibu utapatia, ikiwa ni jambo ulikuwa haujafikiria si lazima ujibu, unaweza kutuambia si kuwa nimefikiria but tunaweza kuuliza swali na uone itakuwa namna gani.

Na mwisho ni lugha, tulisema hii ni Katiba itatoa maoni kwa watu, watu wenyewe watengeneze kwa hivyo tukasema hatuwezi kupatia watu nafasi na tena tuwanyime kwa kusema zungumza kwa lugha fulani, kwa hivyo tunasema uko uhuru kuchagua ile lugha unataka kutumia, unajua itakuwezesha kujieleza sawa sawa. Ukitaka kuzungumza Kiingereza, ukitaka kuzungumza Kiswahili , ukitaka kuzungumza kiteso, uko na uhuru kuchagua ndio ujieleze sawa sawa. Hatutaki urudi nyumbani ukisema nilikuwa nataka kusema hili lakini lugha yenye walisema mimi sikuweza kueleza hii kwa Kiswahili. Sema tu ile lugha unataka, ikiwa ni Kiteso tutapata mtu aweze kututafsiria tuelewe unasema mambo ga/ni.

Mkiingia pale nje kuna mahali ya kuandikisha majina, orodha imewekwa hapo, tutajaribu kufuata hiyo orodha ingawaje kuna wale tutaanza nao kwa programme lakini baada ya hiyo tunarudi kwa orodha, tunafuata vile watu wamekuja, wale wametangulia tunawatangulia. Lakini tena hapo tuna discretion, tunaweza kaa hapa tuone kuna mzee anaanza kuchoka na hatutaki aende na wisdom yake nyumbani, tunaweza patia yeye nafasi turuke wengine. Pengine watoto wanataka kurudi shuleni tunaweza kuwapatia nafasi wamalize waende ama wa mama tunaona wamebaki nyumbani baada ya kutengenezea nyinyi

chakula tena wanataka watangulie huko kutengeneza, tunaweza sema tupatie wa mama priority wamalize waende. So hiyo discretion iko. Kwa hivyo hayo ndio nilikuwa nataka kuleza tuanze mkutano. Asante.

**Com Pastor Ayonga:** Asante Commissioner Mutakha. Hebu hii microphone iwekwe kule. Nadhani mumeshapata maeleze juu ya taratibu ambayo tutafuata na hebu tujaribu kufuata hiyo. ikiwa utakuja hapa mbele na nimekuambia saa yako imekwisha, tafadhali utii. Kutii ni kujali mwenzako, kila mmoja hapa amekuja atoe maoni, jinsi ambavyo Mutakha amesema hakuna mtu anataka arudi amebeba maneno yake kwenda nyumbani. Tumetaka kila mmoja aliye hapa, aliyekuja kusema na aseme na kwa hivyo tunapokuambia time yako inakwisha, ukila time ya mwingine ni kana kwamba unasema wewe sitaki useme, ni mimi tu. Kwa hivyo tusaide kwa kutii. Na ili tuweze kuset, tuweze kuset standard, hebu niite Malaba Town Council, tuone council itatu-treat namna gani. Town council ina memorandum na town council tunawapa dakika dakika tano tafadhali uketi kule nitapenda useme majina yako na useme un-represent council ndipo utumulikie kwa maneno makubwa makubwa yaliyomo katika maandishi yako.

**Cllr. Okiring' John:** Asante Bwana Commissioner. Kwanza kwa kuanza nataka kusema asante kwa kupewa nafasi hii ya kufungua mkutano huu na kwa kupeana memorandum. Majina zangu ni council Okiring' John, mwenyekiti wa hali mashauri la Baraza hili la Malaba. Nina memorandum hapa ambao kama council tulikaa, tukajadiliana tukaona ya kwamba tugawe visehemu, kuna sehemu ambao sisi kama viongozi councillors tuliandikisha hapa na kuna visehemu sisi kama councillors binafsi at individual levels tukaandikisha kwa hivyo kila mmoja wetu nafikiri ana makala yake. But here with me I just want to present what we discussed as a council collectively. Kwea hivyo bwana Commissioner ningependa kusema hapa, lakini tuliingalia sana sehemu za local authorities. Kwanza ningependa kusema kwa citizenship uraia, Bwana Commissioner tuliseme any person born by Kenyan parents or whose father is a Kenya citizen should be an automatic Kenyan citizen. Kwa hiyo nafikiri wanaweza kusikia vile nimesema na tukasema pia a Kenya citizen should be fully protected by the Constitution by having, rights freedom, health and expression and justice.

Tukaenda upande wa political parties, tukasema the new Constitution should regulate the formation of political parties to avoid the creation of tribal parties as it is in the case of today where we have over 40 political parties. Kwa hivyo tulisema ingawa kwa maelezo ya kwamba lazima tuwe na utaratibu ya ku-create political parties kwa sababu haa ukiangalia wakati wa leo kuan wengine wana parties ambazo ni za kabila, pengine mtu mmoja maybe ametoka katika kabla fulani, kwa hivyo lazima tuwe na utaratibu, Constitution wakati huu iwe na utaratibu iwe ina vipengele ambavyovinasema we should have so many parties.

Tukienda katika upande wa executive, tulisema ya kwamba the new Constitution should spell an academic qualification for a presidential candidate and preferably be a university graduate with long experience in Kenyan politics and vast experience in foreign policy and in consolation of his/her track records.

The new Constitution should do away with provincial administration but should keep provision for chiefs to oversee, kuangalia

ule utawala wa chini kabisa kwa sababu provincial administration is very colonial na hata ukiangalia wakati mwingine it has been assisting in the rigging of election kwa sababu ilikuwa inatumika kama chombo cha kuondoa wale hawako katika hiyo ofisi ya juu kuwaondoa wale ambao ni wapinzani wao even if they are very popular.

Bwana mwenye kiti tukaenda tukasema Civic Heads and chairman of local authorities should be vested with the powers to perform the duties of district officer and district Commissioners. Tukasema ya kwamba hawa viongozi, wenye kiti na mayors wape huyo uwezo ya kufanya kazi ambayo district officers, D.Os na DCs walikuwa wanafanya kwa sababu ndio watu wanaelewa kazi na mahitaji ya watu nyumbani. So they will also be accounting officers kama kuna pesa ya serikali ambao imetumwa.

Katika local authorities, tulisema ya kwamba Civic Heads, that is mayors and Chairmen of local authorities should be directly be elected by the people and should have a minimum education of "O" level and with passes in English and Kiswahili. From Experience utaona ya kwamba mtu is very popular amechaguliwa akiingia katika ...amekuwa councillor na tunapoenda katika mikutano hawezi kufuatilia utaratibu wa mikutano. It doesn't matte ukiambia yeye mambo ya orders, ukiambia yeye mambo ya agenda kwa sababu hajaenda shule hajui ni kitugani hata akitaka kusoma minutes hawezi kusoma, hata ukisema a-propose, pengine mambo ya second hajui so qwe want an educated community, leaders ambao wanaweza kuongea kama hata wakitumwa ngambo tu represent the local authorities they should be able to go there na waongee kwa sababu huko hakuna Kiswahili na Kiteso ama Kiluyia so it is English ama Kiswahili. Kwa hivyo tukaona ya kwamba kama hapo itakuwa vizuri itasaidia watu wetu kuongoza local authorities.

Tukasema mayors or chairmen of local authorities wabakie katika ofisi kwa , mayors and chairman of local authority should remain in office for all the five years civic term. In the present Constitution baada ya kila miaka elections. In fact wakati huu kama tungekuwa na elections kwa sababu sasa ya kura hatutakuwa nayo. Miaka mbili haitoshi, tungeona ya kwamba hawa watu wapewe muda huo wote wa miaka tano wakae ofisi tuone kama wanaweza kufanya kazi vizuri kwa sababu miaka mbili haiwezi kutosha.

Other civic candidates Mr. chairmen that is councillors should have a minimum education qualification of O level and kama wengine pia wawe wamepita mihani wa Kiingereza na Kiswahili. Candidates with criminal records or with socvial bad behaviour and debtors to government's institution should be banned. Tuseme wamefungwa kwa sababu ya kuiba pesa pengine ana social weakness pengine huku unasikia leo ana bibi ya fulani sijui nini, I think there should be a body, kuwe na body ambayo inaweza kuangalia na kuona ya kwamba huyu ndio inastahili kusimama kama candidate.

Bwana Commissioner tukasema powers vest with the minister of local government under Cap 265 of the local government should be abolished and local authority should be autonomous. Wakati local authorities are prisoners of the minister of local government kwa sababu hakuna kitu mnaweza kufanya. Kila kitu, approval of estimates, mnapeleka kwa minister, mkitaka

kuajili watu kazi mnapeleka kwa minister, mkitaka nini na nini lazima minister a-approve and this is hata yeye ni mtu politicians kama sisi na isitoshe utaona ya kwamba sometimes mnaweza kupeleka estimates and inakaa, inachukua in fact inachukua karibu zaidi ya mwaka moja so you will have to operate outside the area kwa sababu haijakuwa approved mnafanya kazi bila ya kujua ya kwamba it may not be approved or not. Kwa hivyo tunaona huo uwezo wa minister ipunguzwe, itolewe hata sio kupunguzwa kwa sababu a minister can just dream of a upgrading a local authority, in the dream anaamuka asubuhi anatangaza town fulanai iwe upgraded like ingine ilitangazwa juzi na ingine ilitangazwa jana. So those are random promotions, unaamka tu na kusema Malaba ipewe Municipal council hatutaki, tunasema ya kwamba there should be a body ambayo itaangalia kuona ya kwamba kama inastahili kupandishwa cheo ipandishwe cheo.

Sasa ya mwisho tunasema bwana Commissioner nominations of councillors, members of parliament should be abolished as they are a liability to the tax payers.

Na mwisho kabisa nasema councillors should get their pay from consolidated funds kwa sababu wakati huu bwana Commissioner kuna local authorities zingine for the last five years hawajaweza kulipa councillors wao mishahara. Kwa hivyo kama tunaweza pia kupewa kama Members of Parliament itakuwa vizuri na pia tuwe pensionable otherwise that is the short memorandum I have for these Commission.

**Com Pastor Ayonga:** Thank you very much ngoja kidogo. ulisema political parties tulizo nazo ni nyingi, they are more than 40 lakini haukutuambia unapendekeza zingekuwa ngapi?

**Cllr. Okiring' John:** Asante kwa swali lako, lakini tulipokaa hatukujadiliana ni ngapi lakini tulikuwa tunasema although it is not written here but tukasema anything less than ten itakuwa vizuri. Sio izidi zaidi ya kumi. Asante.

**Com Pastor Ayonga:** Unaweza kuenda kule ukajiandikishe na utuwachie memorandum yako. Next on line ni Teso County Council. Sema majina na uanze.

**Moses Emodo:** I am councilor Moses Emodo, I am 67 years old and I am the Chairman of Teso Town Council. Here Mr. chairman Commissioners, MP, DC Councillors and fellow countrymen. I am happy to welcome you to Teso district and represent the views on behalf of Teso Town Council. We have answered all the question in each article very carefully and gaudily. But Mr. Chairman before I sit down and ... I do humbly ask you to allow me just to polish a few items. Concerning the memorandum I have answered all the articles, we were able to answer all because it was necessary and I have only a few here to polish so that my people can understand.

Defense and national security; we should have a police service not a police force because ukisema force inaonekana unatumia nguvu fulani. Nataka polisi kutokana kwa hali ilivyo iwe service kwa watu ili wafanye na wananchi vizuri ku liko kuwa force

kama forces zingine ambazo zinafanya kazi kwa nguvu kwa sababu tunatakiwa tufanye kazi na polisi pamoja ili tuelewane, tutambue nani ni nani namna hiyo. kwa hivyo jina hii ya force itolewe tuwe na neno service.

Ya pili we want the police service kufanya kazi pamoja na local administration ndio maana ya PR hii relationship ya wananchi na polisi iwe sawa sawa. Kunaforces zingine kama AP, hatujui kazi yao kabisa, haijielezwa katika Katiba kwa sababu wao hawajasomea Sheria katika nchi yetu hii. Lakini pia wanaruhusiwa kwenda kukamata watu, kufanya nini hata hawajui Sheria hii ni nini. Mpaka tena inawabidi wachukuwe kwa wale ambao wanaelewa Sheria hiyo ndio sasa wachukuliwe kotini. Kwa hivyo inakuwa ngumu wao wawe tu wakifanya kazi kama ni kwa ofisi awe tu kwa ofisi na wala sio kwenda kufanya tu, kama ni kwa vita aende vita lakini si kwenda kukamata mwananchi.

Executive; tumependekeza kwamba the post of Provincial Commissioner and District Officers be abolished. Provincial Commissioner's office wote na wadogo wake hapo nchi na D.O.s wote hiyo ofisi itolewe. Hizo ofisi zimekuwa ghali mno bure, tunalia pesa ya kulipa waalimu nini na kumbe pesa inakaa hapo kwa sababu kazi wao wanafanya ni kazi District Commissioner anafanya na ma chifu, kwa hivyo ni duplication ya kazi tu ambao tunafanya hapo. tukitoa hawa pesa nyingi itakuwa inafanya kazi ya nyumbani.

Tena tuliona kwamba presidential decree hapa kenay kuna presidential decree hata Sheria zingine zimefunjwa. Unapata president anaamuka asubui anasema mara moja namna hii namna hii. Presidenyai decree isiwe Sheria, hiyo decree isiwe Sheria kwa maana imeumiza wananchi sana sana, hiyo decree. Kwa sababu anaambiwa maneno anakijaz kwa Baraza, president anatangaza leo hii haitakikani na kesho polisi wanaanza kukamata watu, hiyo si Sheria. Sasa Sheria inababaishwa tu, kwa hivyo tunasema decree is not a law.

Halafu tukasema katika chairmen, our cultural heritage from the Teso people as a community be protected in the Constitution. Sisi kama ni wa Teso, tumeteseka kama si wateso. Katika Kenya sisi tuna utamaduni wetu, kuna viti vingi ambavyo tunafanya pendine zingine zinalingana katika utamaduni wa waafrika. Zingine zinalingana, zingine hazipo, tunaona zingine zimepuuzwa. Tukianza kufanya namna hii, mtu pengine kama Coast anakuja anaanza kuchekea mtoto pengine yuko nyuma sana na haelewi sisi wateso tabia yetu ni gani. Tunataka hiyo iheshimiwe na kabla zingine kzama utamaduni yetu kama sisi unajua unapata ni mtu kutoka pengine kwa Utanalii kule akipata mtoto akinywa na calabash yake anaanza kucheka ati huyu Mteso ni wa chini sana huyu na kumbe hiyo ni tabia yetu, tumekuwa na hiyo kwa miaka mini, hatutaki hiyo ipuuzwe na mtu mgeni ambaye nakuja hapa, iheshimiwe. Kwa hivyo mila zetu kama traditional; food and drinks ziheshimiwe, also traditional traditional songs ziheshimiwe, traditional marriages and languages kwa sababu sisi tumeona kila chochote ambacho tunaweza fanya kuna Sheria pale. Kama kabla zingine, kama ni kuoja si lazima tuweke makaratasi kwa harusi, kuna sherehe ya kuoja kwa Mteso, ambayo watu wanakuja, watasidikiza msichana mpaka hapa. sasa sherehe hiyo pengine kuna kunywa na kukula ambayo sasa inakataliwa, hatuwezi kukunywa, tumeambiwa tu kwenda kwa bar, tumeambiwa ati pombe ya kienyeji ambayo inatanguliwa tangu zamani, hiyo si pombe. Hii iko commercialized kabisa ti Mteso lazima aende kwa bar na Mteso mwenyewe huyo hawezi kwenda kwa

bara, kwa sababu kama ni ulevi pombe yote inaleweshwa. Hii ya bar kama ambayo ni commercial pia hiyo itupiliwe mbali na hii pia itupiliwe mbali.

Sheria iwekwe kwamba pombe ni pombe, na kama kuna pombe kama ya kienyeji ambayo inatengenezwa na wa Teso tangu zamani, serikali ina ruhusa kuleta mtaalamu kuangalia kama hiyo pombe ni mbaya ama namna gani ili waendelee na hiyo na wale wa chini waendelee na hiyo kuliko kusema bar peke yake, bar hiyo maana pombe ya kienyeji imekatazwa. Kwa hivyo tunaomba... (interjection).

**Com Dr. Nunow:** Kwa ufupi unasema utamaduni wa kila kabila uheshimiwe na makabila ingine.

**Moses Emodo:** Yeah.

**Com Pastor Ayonga:** You have made your point, enda point ingine.

**Moses Emodo:** Ingine sasa about local authority; katika Kenya local authority haina nguvu sana. Unapata kama council, kama nimi Chairman sina ruhusa ya kuandika na kufuta mfanyi kazi. Sheria zote kwa minister, sasa unaona wewe Chairman ya nini ambao huna uwezo wa kufuta na kuandika. Kwa hivyo uwezo upewe kwa council ili mwenye kiti ama mayor awe na uwezo wa kufuta na kuandika.

Ya mwisho ni juu ya (inaudible) sisi kama Wateso tuko kwa border ya Kenya na Uganda watoto wengi wako Uganda, watoto wengi wako Kenya utapata wanawake wengi ambao ni wa Uganda wameolewa hapa na wengi wa Kenya wameolewa kule. Na kule Uganda wanawake wetu wakienda kule ni rahisi sana kukubaliwa kwamba ni wanawake wa kule hata kuandikishwa. Lakini wa Uganda wakija hapa huwa ngumu sana, kuna wanawake wamekwa wazee mpaka saa hii hawawezi kupiga kura, hawawezi kuenda Nairobi maana hawana kipande, wananyimwa mwanamke hata ni mzee. Pengine sisi tunasema hivi, mwanamke akiolewa, cheti kipatikane cha yeye kuolewa katika district yetu hata kama ni kutoka Uganda, Tanzania, apate chetu hicho. Cheti hicho pengine mda fulani ufike ndio awe sasa mwananchi. Sasa tunaomba hiyo iwekwe kwa sababu tunaumia sana katika border, watu wengi hawapigi kura kwa sababu three quarters ya wanawake ni kutoka Uganda. Kwa hivyo tunaumia na hawa hawafanyi kazi yoyote. Kwa hivyo njia ipatikane kama ambayo ninasema, barua kwanza na local iletaye barua kwa DC iandikishwe huyu ameolewa na sasa hiyo itumiwe pengine kupata kipande, na aruhusiwe kupiga kura na kazi iende. Asante. Kwa hivyo ni hayo tu nasema asante sana.

**Com Mutakha Kangu:** Barua unasema ya ndoa, itolewe na DC ama wapi na umeshasema ofisi ya DC iende, sasa nani kwa administration atatoa barua.

**Moses Emodo:** Sijasema ofisi ya DC itolewe, katika provincial administration ninasema tu Provincial Commissioner's office na

District Officer, ni DO na PC, ofisi zao na watu wake wote wao watolewe. Wakitoka Nairobi mpaka hapa iende kwa DC halafu chiefs na assistant chiefs.

**Com Dr. Nunow:** Bwana Chairman ningeopenda kufualtilia hiyo mambo ya citizenship. Kweli ni matatizo ambayo uliyataja na ulisema kwamba mume kutoka Kenya akioa mke kutoka ngambo hawezi kupatiwa shahada ya hiyo marriage halafu baada ya muda fulani aweze kupatiwa documents za mwananchi hapa. muda gani ungeona inafaa kwamba mke akiwa ameolewa nchini angeweza kupewa kitambulisho na passport.

**Moses Emodo:** Kuna utamaduni wa kuolewa, kuna mahali unachukuliwa kule na kule ndio watu wa Uganda wanajua msichana ameolewa Kenya, kuandikisha harusi, kama ni arusi, kama nikitamaduni aende kwea chief ama aende kwa DC halafu aende kwa DC halafu aandikishwe.

**Com Pastor Ayonga:** Ngoja, tafadhali nyinyi msimuingilie. Kitu ambacho Dr. Nunow amekuuliza ni muda gani? Ni mwaka mmoja, miaka mbili, miaka mi tatu, mambo hayo ya halalishwe au we have to have time factor.

**Moses Emodo:** Mimi napendekeza miaka mbili inatosha.

**Com Pastor Ayonga:** Miaka miwili, basi umejibu. Nenda ujiandikishe kule mzee na utuwachie hiyo memorandum sasa imekuwa mali yetu.

Nest ni Maendeleo ya wanawake. Mama una maadishi na una dakika tano, tunataka tu utumulikie ni nini kubwa kubwa iko hapo ndani. Kwanza useme majina yako na kikundi cha Maendeleo unachosimamia.

**Roselyn Ashabete:** Mr. Commissioner Sir, Chairman of today's meeting and all your team, may I welcome to Teso. My names are Roselyn Ashebete, I have stood for Maendeleo ya Wanawake and also Women in Teso. The memorandum I am going to read is gender sensitive and I hope I will be excused if some issues will be very touching to our brothers.

In the preamble; I am only going to highlight a few items because I have very little time, the others I will give for record.

In the preamble the new Constitution should highlight the marginalisation of vulnerable groups such as communities who live along Kenyan borders like those in Teso, women, the youth, minorities from all tribes and the aged persons and also persons with disabilities. If this one is included in the preamble it is going to be good. in the vision there should be equality of all Kenyans, of all citizens of Kenya regardless of race, ethnicity, gender, class, creed or political affiliation.

In the directive principles there should be values and these should include human dignity and equality, gender equality, and non discrimination. There should be respective for human rights. The rights of women and the child and especially the girl child. And

also there should be affirmative action to achieve this equality.

In the Constitutional Supremacy; we note that neither parliament nor the executive nor the judiciary should have any powers whatsoever to amend the Constitution of Kenya. this should be done in a referendum and these areas should include the presidential term of office, citizenship among others.

In citizenship the element of gender discrimination with regard to citizenship in the current Constitution, especially reference section 90 &91 is noted with regrets. We the women of Teso recommend as follows:-

- (1) There should be automatic citizenship to an child born in Kenya or out of Kenya to one of the Kenyan parents, be it a mother or a father.

In defense and national security; there should be equal opportunities and gender balance in employment within the armed forces.

In political parties Kenya shall be a multiparty state. The Constitution should control and regulate the formation and number of political parties in Kenya not less than two and not more than five. Every political party should allow 35% elective positions reserved for women.

Structures and system of government; the current systems of government has failed to server the social, economic and political need and aspirations of the women of Teso and Western as a whole. So the present system is over centralized and has got power and the power should be devolved thus allowing room for better participation of both women and all ethnic groups in the exercise of governance.

In the legislature; I should say through affirmative action women should occupy 50% of the nominations positions ion parliament. The personal conducts of the candidates that is a Councillor or an MP an elective post shall be vetted by an ethics committee appointed by the electoral Commission.

In the executive; the office of the executive is a Constitutional office, not the office of a clan a tribe or a set of friends.

Participatory governance; the provincial administration is a vestige of the colonial powers. It is expensive and duplicates the roles of elected local leaders. For that we recommended even the selection of the police should be done locally by the community because there is a lot of corruption and members and the public and the communities are made to pay unnecessary money for posts that should have been freely given.

**Com Pastor Ayonga:** Please we don't entertain others speaking when a person is presenting. Whether you agree or you don't agree please be quite.

**Roselyn Ashabete:** In the judiciary, the current system is corrupt, insensitive to the poor and incompetent, given the long period of time it takes to clear cases, justice delayed is justice denied. It is true of the experience of women of Teso. There is simply no justice.

The judiciary should reconceptualize to address the needs of all Kenyans in particular the poor, women the disabled, the marginalized and minors. We the women need a complete change from the present colonial and oppressive ineffective system that has denied us our rights. The Constitution should ensure there are checks and balances to ensure the independence of the judiciary and should also control and manage for the people, the smooth and effective operations of the judiciary.

In local government, other points have been said but I should say the Constitution will through affirmative action ensure 35% representation of women on all local authorities. The violence, bribery gang terrorism during election campaign should be Constitutionally outlawed and those governing the exercise be strictly controlled by the electoral Commission.

On the bill of rights; the basic rights, there should be gender equality and in deed the equality of all citizens of Kenya to be entrenched in the Constitution as a basic fundamental rights. Current areas which experience inequality include disability, ethnicity, and the change of identity cards after divorce is a factor that has really affected women because they are never done in a better way, they take very long.

To finish up, there are also issues in another smaller memorandum which the people discussed and the women came out with. About education; free education to children, about health facilities which should actually be free because most women are not able to afford the prices that are offered or the sharing systems, so many children keep on dying and then the poverty. If we help women to grow, we shall help our country to grow.

Power and decision making, women should be involved, cases of rape that is why we talked about the judiciary being a bit silent so rape cases are dealt with very mildly as if nothing has happened, family violence, men kill their women and nothing is done and yet the law is supposed to protect women, family land, when the man dies the woman is chased away, it becomes a problem so women should be protected. Family property when the man dies, the woman should be allowed to stay in the compound and not be inherited because this are days of AIDS and when you refuse they chase you away. So we want women inheritance abolished. Thank you Mr. Commissioners sir.

**Com Pastor Ayonga:** Thank you mama for your concerns. You have any questions?

**Com Mutakha Kangu:** You said that 50% of the nominated members of parliament should be women. Right now we have only 12 nominated members of parliament, 50% of that would be six, you think that is sufficient for women in the whole

country?

**Roselyn Ashabete:** I think here I am refereeing to the total number of all the MPs present. Right now there is very poor representation of women and if in any way they have to make anything, they really have to be many and they work as a group. The few are not able to represent women fully.

**Com Mutakha Kangu:** So you want 50% of the entire House.

**Roselyn Ashabete:** Yes.

**Com Mutakha Kangu:** Now what mechanisms will you want used to get these 50 % because the experience across the border in Uganda in Uganda is that they have created district seats for women so women contest in the district so you elect an MP for a constituency but you also elect a woman MP for the district. Now what mechanisms do we use in Kenya to secure these 50% for women.

**Roselyn Ashabete:** Surely Uganda has done well and we envy them. If in Kenya we will follow sets and give a directive in the new Constitution that smaller smaller areas of every constituency or even division, should have elective positions for women to represent them in the higher offices. These will help to elevate the present problems that the women are facing because if we only are able to take one woman even in a constituency, it should be able to come and listen to our problems but a man in his own capacity cannot know all the problems of a woman.

**Com Pastor Ayonga:** I thought mama that these men leave with the women.

**Roselyn Ashabete:** Yes but Commissioner they live with us, but you see they don't understand us.

**Com Pastor Ayonga:** Why don't you make it easier for them to understand?

**Com Pastor Ayonga:** We are really trying to lobby and sweet talk them so that they don't keep on oppressing us, we need to be set free.

**Com Dr. Nunow:** Madam, I would like to ask you a bit of clarification, on recruitment of people into civil service particularly you made particular reference to the security forces and you said that should be brought to the lower levels where the people are. At what level do you recommend that the recruitment into the armed forces and the police be conducted. At the location, sub location, division or the district level. Which level will you consider appropriate.?

**Roselyn Ashabete:** I would have preferred the divisional level because when we conduct it in the district and we are given very few chances it becomes hard and especially the present system where you find, I am not afraid to say there is a lot of corruption because when you have to take a child or a boy to be taken in the armed forces or in the police or an AP. They demand a lot of money from us. it is almost impossible even the boys who pass are not get this chances.

